JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2023

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2023

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI .......... iv

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI .......... 3

2.1 Sehemu A: Kuchagua Jibu Sahihi na Kuoanisha .......... 3
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi .......... 3
2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu .......... 12
2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi .......... 15
2.2.1 Swali la 3: Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W) .......... 15
2.2.2 Swali la 4: Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini .......... 18
2.2.3 Swali la 5: Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu .......... 22
2.2.4 Swali la 6: Qur'an .......... 26
2.2.5 Swali la 7: Sunna na Hadithi .......... 28
2.2.6 Swali la 8: Historia Katika Uislamu. .......... 34
2.2.7 Swali la 9: Bara Arab Zama za Jahiliyyah Karne ya 6 A.D .......... 37
2.3 Sehemu C: Insha .......... 39
2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu .......... 39

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA .......... 44

4.0 HITIMISHO .......... 45

5.0 MAPENDEKEZO .......... 45

Kiambatisho cha Pekee .......... 46

Uchambuzi wa Ufaulu wa Wanafunzi katika Mada .......... 46

## DIBAJI

Uchambuzi huu unaonesha majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2023 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Uchambuzi huu ni mrejesho kwa wadau wa Elimu kuhusu viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika upimaji wa somo hili na sababu mbalimbali zilizochangia katika ufaulu huo.

Taarifa hii imebainisha sababu zilizochangia wanafunzi hao kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Sababu zilizowawezesha baadhi ya wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada zilizopimwa na kuelewa matakwa ya maswali yaliyoulizwa. Aidha, uchambuzi huu umebaini kuwa wanafunzi walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika mada mbalimbali za Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali katika mada husika.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha walimu, wanafunzi, wazazi, watunga sera na wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Endapo mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yatazingatiwa, ni imani ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika uandishi wa taarifa hii.

**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) Novemba 2023 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika wa Kidato cha I na II ulioandaliwa mwaka 2012.

Maswali katika upimaji huu yaliandaliwa kutoka katika mada kumi ambazo ni: *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi, Bara Arab zama za Jahiliyyah, Fiqh, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Historia katika Uislamu* na *Kumjua Mwenyezi Mungu*. Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali saba (3, 4 ,5, 6, 7, 8 na 9) na sehemu C ilikuwa na swali moja (10). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote kumi (10).

Wanafunzi waliosajiliwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2023 walikuwa 95,223 kati yao wanafunzi 87,502 sawa na asilimia 91.89 walifanya upimaji. Idadi hiyo inaonesha kuwa kuna ongezeko la wanafunzi 2,282 ikilinganishwa na wanafunzi 85,220 waliofanya upimaji wa somo hilo mwaka 2022. Kati ya wanafunzi 87,502 waliofanya upimaji mwaka 2023, wanafunzi 59,621 (68.32%) walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya wanafunzi hao ikilinganishwa na mwaka 2022.

**Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu kati ya Mwaka 2022 na 2023**

| Mwaka | Asilimia ya Ufaulu | Madaraja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2022 | 48.77 | 51 | 420 | 9,645 | 31,083 | 43,271 |
| 2023 | 68.32 | 200 | 1,586 | 21,586 | 36,249 | 27,651 |

Takwimu katika Jedwali Na.1 zinaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2023 kimepanda kwa asilimia 19.55 ikilinganishwa na mwaka 2022. Aidha, idadi ya wanafunzi waliofaulu kwa daraja A mwaka 2023 imeongezeka mara tatu zaidi ya mwaka 2022, wakati idadi ya wanafunzi waliopata daraja F imepungua kwa takribani nusu ya idadi ya mwaka 2022.

Taarifa hii imechambua majibu ya wanafunzi katika kila swali kwa kuzingatia matakwa ya swali husika, majibu sahihi ya swali hilo na yale waliyotoa wanafunzi katika swali hilo. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa ili kuonesha namna wanafunzi walivyojibu maswali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili wanafunzi katika kujibu kila swali na kiwango cha ufaulu katika mada mbalimbali zilizopimwa. Aidha, madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu katika Elimu ya Dini ya Kiislamu**

| Alama | Daraja | Maoni |
|---|---|---|
| 75 – 100 | A | Vizuri Zaidi |
| 65 – 74 | B | Vizuri Sana |
| 45 – 64 | C | Vizuri |
| 30 – 44 | D | Inaridhisha |
| 0 – 29 | F | Dhaifu |

Jedwali Na. 2. linaonesha kuwa daraja la juu zaidi la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la chini zaidi ni F. Pamoja na kuwa na madaraja matano ya ufaulu kama yalivyooneshwa, taarifa hii itatumia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu utakuwa dhaifu ikiwa wanafunzi waliofaulu katika swali ni kati ya asilimia 0 hadi 29. Ufaulu utakuwa wa wastani ikiwa waliofaulu swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu utakuwa mzuri ikiwa ni asilimia 65 hadi 100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI


### 2.1 Sehemu A: Kuchagua Jibu Sahihi na Kuoanisha

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambayo mwanafunzi alipaswa kujibu maswali yote. Swali la kwanza lilikuwa ni la kuchagua jibu sahihi katika vipengele kumi (i) – (x) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama moja (01). Swali la pili lilikuwa ni la kuoanisha, ambalo lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v). Swali hili lilikuwa na alama tano (05) sawa na alama moja (01) kwa kila kipengele. Hivyo, sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 15.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi

Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo manne waliyopewa (A, B, C na D) kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kisanduku. Swali hili lilipima ngazi mbalimbali za umahiri katika mada za *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi na Bara Arab zama za Jahiliyyah.*

Wanafunzi wote 87,502 (100%) walijibu swali hili. Kati yao wanafunzi 68,239 (77.98%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi 10,410 (11.90%) walipata alama 7 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, wanafunzi 8,853 (10.12%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeainishwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1.*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 89.87 kati ya wanafunzi wote walichagua majibu sahihi na kupata alama 3 hadi 10. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali zilizounda vipengele kumi vya swali hilo.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele ni kama ifuatavyo:

Kipengele (i), mwanafunzi alitakiwa kubaini amali inayotoa nafasi kubwa kwa mtu kuwa mchamungu zaidi kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka amali muhimu inayotoa nafasi kubwa ya mtu kuwa mchamungu kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Wanafunzi weledi katika dhana ya Elimu waliweza kuchagua jibu sahihi *C Kuzama kielimu katika fani mbalimbali.* Aidha, wanafunzi hao walikumbuka kuwa elimu ni msingi mkuu unaomuwezesha mja kutekeleza amali zote kwa ufanisi hatimae kumfikisha katika daraja la uchamungu.

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua vipotoshi A *Kusali katika msikiti wa Makkah,* na D *Kusimama usiku katika msikiti wa Aqsa.* Wanafunzi hao walichanganya utukufu na daraja za malipo ya ibada katika misikiti hiyo katika kuufikia uchamungu na kushindwa kuelewa kuwa kutafuta Elimu ni msingi wa kwanza wa kutekeleza ibada zote. Wengine walichagua kipotoshi B *Kufunga Sunnah katika miezi mitukufu* kwa kuwa dhana ya uchamungu ni malengo ya wazi ya ibada ya Funga. Hata hivyo wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa ibada hiyo ya Funga kama zilivyo; ibada nyingine, haiwezekani kutekelezwa ipasavyo bila ya elimu.

Katika kipengele cha (ii), mwanafunzi alitakiwa kubainisha ishara inayomtambulisha Muislamu kwa watu wengine katika jamii. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa dhana sahihi ya mtu kuwa Muislamu. Wanafunzi hodari walionesha kuelewa vema dhana hiyo na kuchagua jibu sahihi A *Tabia na mwenendo mwema.* Wanafunzi hao walielewa vema kuwa tabia njema ndio kitambulisho cha kwanza cha Muislamu wa kweli kwani jambo hilo limepewa hadhi kuwa zaidi ya nusu ya mafundisho ya Uislamu na ndio msingi aliyokuja nao Mtume Muhammad (S.A.W).

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua kipotoshi *B, Majina mazuri ya Kiarabu,* jambo ambalo linaashiria kueleweka vibaya kwa jina la Uislamu na kuchanganywa baina ya tamaduni za Kiarabu na Uislamu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kuelewa kuwa Uislamu sio Uarabu, hivyo kuwa na jina la kiarabu hakuoneshi anuani sahihi ya Uislamu wa mtu. Wengine walichagua kipotoshi C *Mavazi na mwendo wake* ambalo pia ni dhana inayoonesha kueleweka vibaya kwa Uislamu, ambapo baadhi ya watu uhusianisha aina fulani (maalumu) ya mavazi kuwa ni vazi linalomtambulisha Muislamu. Jambo hilo sio sahihi kwa sababu Uislamu umeweka kanuni zinazoongoza namna ya kuvaa na haujataja vazi maalumu kwa sababu unatambua kuwepo kwa utofauti baina ya mitindo na mitazamo ya kijinsia baina ya jamii mbalimbali duniani.

Kadhalika, waliochagua kipotoshi D *Kutumia muda mrefu msikitini*, nao walishindwa kuelewa kuwa anuani ya Muislamu inajengwa kwa asilimia chache akiwa msikitini na asilimia kubwa zaidi katika miamala anayofanya na watu wengine nje ya msikiti. Hivyo, kutumia muda mrefu sana msikitini sio ishara toshelevu kubainisha Muislamu wa kweli.

Kipengele cha (iii), mwanafunzi alitakiwa kubainisha maana sahihi ya Nisaab kwa mujibu wa elimu ya Zaka. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa dhana ya Nisaab kama inavyotumika katika utoaji wa Zaka. Wanafunzi mahiri katika mada ya Zaka walielewa vema kipengele hicho na kuchagua jibu sahihi C*, Kiwango maalumu cha mali inayostahiki kutolewa Zaka.* Wanafunzi hao walielewa kuwa Zaka inatofautiana kati ya aina mbalimbali za mali hivyo na kila mali ina kiwango chake tofauti cha kuanza kuhesabiwa katika utoaji.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya Zaka, hivyo walichagua vipotoshi A *Kiwango cha juu cha mali inayostahiki kutolewa Zaka,* B *Kiwango cha kati cha mali inayostahiki kutolewa Zaka* na wengine walichagua kipotoshi D *Kiwango cha mwisho cha mali inayostahiki kutolewa Zaka.* Wanafunzi hao wote walishindwa kuelewa kuwa Nisaab sio kipimo kinachofafanuliwa kwa upande mmoja (juu, kati au mwisho) kwakuwa mali zinazojuzu kutolewa Zaka zinatofautiana, hivyo tafsiri inayotosha kufafanua Nisaab kwa usahihi ni kuwa kiwango maalumu cha mali kinachostahiki kutolewa Zaka.

Katika kipengele cha (iv), mwanafunzi alitakiwa kubaini jambo linaloashiria uzuri wa dini ya Uislamu kwa kuzingatia wepesi wa mafunzo na taratibu zake, ambapo mwanafunzi alipaswa kukumbuka ruhusa iliyotolewa katika Uislamu katika kutekeleza ibada ya Sala tano. Wanafunzi mahiri katika mada ya Sala walichagua jibu sahihi B *Kukusanya swala kwa mgonjwa*. Wanafunzi hao walielewa kuwa katika Uislamu miongoni mwa waliopewa ruhusa ya kukusanya na kupunguza rakaa za Sala ni wagonjwa na wasafiri.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi katika kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya Elimu ya Sala, hivyo walishindwa kubaini jibu sahihi. Wanafunzi hao walichagua vipotoshi A *Kusamehewa Sala kwa msafiri,* C *Kusamehewa Sala kwa mgonjwa* na wengine D *Kusamehewa Sala kwa mjamzito.* Aidha, wanafunzi hao walionesha kutokuwa na elimu sahihi kuhusu uzuri wa Uislamu kwani makundi hayo hayapo katika waliosamehewa kutekeleza ibada ya Sala.

Kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kubaini sababu ya kusisitizwa sana kwa Sala za Sunnah katika Uislamu, ambapo katika kipengele hiki mwanafunzi alipimwa kiwango cha uelewa wake kuhusu umuhimu wa Sala za Sunnah. Wanafunzi waliokuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu Sala za Sunnah waliweza kuchagua jibu sahihi D *Ni njia ya kufikia uchamungu kwa wepesi.* Wanafunzi hao walielewa vema nafasi ya Sala za Sunnah kwa Muislamu na kuonesha nafasi hiyo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi baadhi yao walichagua kipotoshi A *Zinaongeza thawabu kwa waumini,* jambo ambalo ni sahihi lakini sio sababu ya kusisitizwa kwa Sala hizo. Wengine walichagua B *Zinamuwezesha mtu kuwafikia maswahaba* ambalo halikuwa jibu sahihi kwa sababu hakuna juhudi ambayo Muislamu wa sasa ataifanya akawafikia Maswahaba wa Mtume (S.A.W). Kadhalika, baadhi yao walichagua kipotoshi C *Zinasababisha watu kufanana na Mitume,* ambalo pia halikuwa jibu sahihi kwani kufanana na Mitume (A.S) ni jambo la jumla sana na sio Mitume wote walikuwa na Sunnah hizo.

Katika kipengele cha (vi), wanafunzi walitakiwa kubainisha jina ambalo halitambulishi Suratul Fat-ha katika orodha ya majina waliyopewa. Kipengele hiki kilipima umahiri wa mwanafunzi kuelewa maana ya majina mbalimbali ya Qur'an. Aidha, wanafunzi mahiri katika mada ya Qur'an

walitambua jina hilo na kulibainisha kwa kuchagua herufi D *Al-Bayaana.* Jina hilo lenye maana ya *kilichofafanuliwa au kilichowekwa wazi* halikuwa mahususi kwa Surat Fat-ha bali linaitambulisha Qur'an yote kwa sababu ya maana yake.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kukosa maarifa kuhusu maana ya majina ya Suratul Fat-ha. Baadhi ya wanafunzi hao walichagua kipotoshi A *Faatihatul- kitaab* lenye maana ya ufunguzi wa kitabu cha Qur'an*,* ambalo ni jina sahihi la Sura hiyo kwakuwa sura hiyo ni ya kwanza kabisa katika Qur'an. Wengine waliochagua kipotoshi B *Ummul- kitaab* lenye maana ya mama wa kitabu, ambalo pia ni katika majina ya Sura hiyo kwakuwa sura hiyo ni muhtasari wa maudhui yote yaliyomo katika Qur'an. Vile vile walikuwepo waliochagua kipotoshi C *Assab' ul - Mathaan* lenye maana ya aya saba zenye kurejewa, kwakuwa sura hii ni nguzo katika kila rakaa ya Sala hivyo inakuwa ni sura yenye kusomwa mara nyingi zaidi katika maisha ya Muislamu. Kwa ujumla wanafunzi waliokosa katika kipengele hiki walionesha wazi kuwa walikosa maarifa kuhusu mada ya Qur'an hasa katika kutambua maana ya majina mbalimbali ya Surat Fat-ha.

Kipengele cha (vii), mwanafunzi alitakiwa kubaini hukumu ya Nuun Sakna inapokutana na *Bee* (بَ) yenye *Fat-ha*, ambapo mwanafunzi alipimwa uelewa wa hukumu mbalimbali za usomaji wa Qur'an. Aidha, jibu sahihi katika kipengele hiki lilipaswa kuwa *Iqlaab,* lakini jibu hili lilikosekana katika orodha ya majibu yaliyopendekezwa, hivyo majibu yote hayakuwa sahihi.

Majibu yaliyowekwa katika kipengele hiki yalikuwa kama ifuatavyo; Herufi A *Idghaam* ambapo hukumu hii inajitokeza katika herufi sita ambazo ni: *Yee* (ى) *Ree (ر), Miim (م), laam (ل), Wau (و)* na *Nuun (ن)* zinapokutana na *Nuun sakna au Tanwiin.* Herufi B *Idghaam yenye Ghunna na* herufi C *Idghaam pamoja na Ghunna* hukumu hii inajitokeza katika herufi nne ambazo ni: *Yee (ى), Miim (م), Wau (و)* na *Nuun (ن)* zinapokutana na *Nuun sakna au Tanwiin.* Wakati herufi D *Idghaam Mutamaathilayn* hupatikana zinapokutana herufi mbili zinazofanana ikiwa ya mwanzo ina *Sakna,* mfano herufi *Bee (بْ)* na *Bee (بَ)* ikiwa *Bee* ya mwanzo ina *Sakna* au herufi *Daal* (دْ) na *Daal (دَ),* ikiwa *Daal* ya mwanzo ina *Sakna*.

Kipengele cha (viii); Mwanafunzi alitakiwa kuonesha kipindi ambacho ilijitokeza kazi ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi za Mtume (S.A.W) iliyofanywa na wanazuoni sita mashuhuri. Katika kipengele hicho mwanafunzi alipimwa uwezo wa kukumbuka vipindi mbalimbali vya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi. Aidha, wanafunzi mahiri katika mada ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi za Mtume (S.A.W) waliweza kuchagua jibu sahihi *D Wakati wa Tabi'i tabiin*, kwakuwa walikumbuka vema kazi hizo kubwa zilizofanywa na wanafunzi wa wanafunzi wa Maswahaba.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu vipindi mbalimbali vya uandishi wa Hadithi na kazi zilizofanywa. Baadhi ya wanafunzi hao walichagua kipotoshi A *Wakati wa Mtume (S.A.W)* ambacho sio sahihi kwani katika kipindi hiki hapakuwa na uandishi mkubwa wa Hadithi na wala haikuonekana haja ya uchambuzi kwa kuwa Mtume (S.A.W) mwenyewe alikuwepo. Wengine walichagua herufi B *Wakati wa maswahaba*, ambalo pia halikuwa jibu sahihi kwani kipindi hiki nacho hakikuwa na uandishi mkubwa zaidi ya juhudi ya sahaba mmoja mmoja kama vile Ali (R.A) ambae aliandika Sahifa yake (pamphlet). Ama waliochagua kipotoshi C *Wakati wa Tabiina,* walisahau kuwa pamoja na juhudi zilizofanywa na wanafunzi wa maswahaba katika uandishi hapakuwa na juhudi kubwa ya kiuchambuzi na uhakiki wa Hadithi kwani bado walikuwepo maswahaba wengi wakurejewa.

Katika kipengele cha (ix), mwanafunzi alitakiwa kubainisha daraja la hadithi iliyokubaliwa na maimamu wanne isipokuwa Bukhari na Muslim. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua daraja mbalimbali za Hadithi za Mtume (S.A.W). Wanafunzi mahiri katika mada ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi walichagua herufi ya jibu sahihi C *Daraja la saba* kwa kuwa ndilo daraja stahiki kwa Hadithi hizo katika ngazi za ithibati.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hicho waliashiria kukosa maarifa ya kutosha katika mada ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi za Mtume (S.A.W). Baadhi ya wanafunzi hao walichagua kipotoshi A *Daraja la tatu,* jibu hili halikuwa jibu sahihi kwani Hadithi ya daraja la tatu ni ile iliyopokelewa na Imam Muslim pekee. Wengine walichagua kipotoshi B *Daraja la tano,* ambalo pia halikuwa sahihi kwani daraja hilo ni kwa Hadithi zilizozingatia vigezo vya uchambuzi vilivyowekwa na Imamu Bukhari pekee. Vile vile wapo waliochagua kipotoshi D *Daraja la*

*nane,* ambalo kadhalika halikuwa jibu sahihi kwani hakuna Hadithi za daraja hilo kwakuwa mwisho wa daraja za Hadithi za Mtume (S.A.W) ni saba.

Kipengele cha (x); mwanafunzi alitakiwa kuonesha funzo linalotokana na Mtume Muhammad (S.A.W) kulingania Uislamu watu wa Makka kwa siri katika miaka mitatu ya mwanzo ya utume wake. Kipengele hiki kilipima umahiri wa kuelewa Historia ya Uislamu kipindi cha Makkah. Wanafunzi mahiri katika mada ya Bara Arab Zama za Jahiliyah waliweza kujibu kipengele hiki kwa usahihi na kuchagua jibu sahihi C. *Makafiri hawawezi kukubali kuona Uislamu unakuwa.* Wanafunzi hao walielewa vema makusudio ya kipengele hiki hivyo waliweza kubaini jibu ambalo lilitosheleza zaidi.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Historia ya Uislamu kipindi cha Makkah, hivyo baadhi yao walichagua kipotoshi A *Muhimu kuwa wasiri mwanzo wa harakati za daa'wa.* Hoja hii haikuwa sahihi kwakuwa iliendelea kusherehesha swali lililoulizwa badala ya kutoa majibu. Wengine walichagua kipotoshi B, *Ili kazi* ya *kulingania watu ifanikiwe lazima ifanywe na Mitume,* ambalo pia halikuwa jibu sahihi kwa sababu kazi ya kulingania ni ya wote. Wengine walichagua kipotoshi D*, Ili Waislamu wafanikiwe lazima kuficha mbinu za* daa'wa, jibu hili pia sio sahihi kwa sababu halina mantiki. Hivyo, wanafunzi hao hawakuelewa kusudio la kipengele hiki, ambalo linaeleza kuwa: Miongoni mwa mafunzo ya kulingania kwa siri ni kuwa makafiri hawawezi kukubali Uislamu kukuwa. Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 1 na kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hilo.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Amali gani inatoa nafasi kubwa kwa mtu kuwa mchamungu zaidi kwa mujibu wa Uislamu?

A Kusali katika msikiti wa Makkah
B Kufunga Sunnah katika miezi mitukufu
C Kuzama kielimu katika fani mbalimbali
D Kusimama usiku katika msikiti wa Aqsa

[ C ]

(ii) Muislamu wa kweli anaonekana na wengine katika jamii kwa ishara gani?

A Tabia na mwenendo mwema
B Majina mazuri ya kiarabu
C Mavazi na mwendo wake
D Kutumia muda mrefu msikitini

[ A ]

(iii) Ufafanuzi gani unatosheleza kutoa maana sahihi ya Nisab katika elimu ya Zaka?

A Kiwango cha juu cha mali inayostahiki kutolewa Zaka
B Kiwango cha kati cha mali inayostahiki kutolewa Zaka
C Kiwango maalumu cha mali inayostahiki kutolewa Zaka
D Kiwango cha mwisho cha mali inayostahiki kutolewa Zaka

[ C ]

(iv) Jambo gani linaashiria uzuri wa dini ya Uislamu kwa kuzingatia wepesi wa mafunzo na taratibu zake?

A Kusamehewa Sala kwa msafiri
B Kukusanya Sala kwa mgonjwa
C Kusamehewa Sala kwa mgonjwa
D Kusamehewa Sala kwa mjamzito

[ B ]

(v) Kwa nini Sala za Sunnah zimesisitizwa sana katika Uislamu?

A Zinaongeza thawabu kwa waumini
B Zinamuwezesha mtu kuwafikia Maswahaba
C Zinasababisha watu kufanana na Mitume
D Ni njia ya kufikia uchamungu kwa wepesi

[ D ]

(vi) Surat-Fat-ha inajulikana kwa majina mbalimbali **isipokuwa**

A *Faatihatul-kitaab* B *Ummul-kitaab*
C *Assab'ul-Mathaan* D *Al-Bayaana*

[ D ]

(vii) Katika usomaji wa Qur'an herufi *Nuun* yenye *Sakna* inapokutana na *Bee* (ب) yenye *Fat-ha* inasababisha kupatikana kwa hukumu gani?

A *Idghaam* B *Idghaam* yenye *ghunna*
C *Idghaam* pamoja na *ghunna* D *Idghaam Mutamaathilayn*

[ D ]

(viii) Kazi ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi iliyofanywa na wanazuoni sita mashuhuri ilijitokeza katika kipindi gani?

A Wakati wa Mtume (SAW)
B Wakati wa Maswahaba
C Wakati wa Tabiina
D Wakati wa Tabi'i tabiin.

[ D ]

(ix) Hadithi iliyokubaliwa na Maimamu wanne isipokuwa Bukhari na Muslim inapewa daraja gani?

A Daraja la Tatu B Daraja la Tano
C Daraja la Saba D Daraja la Nane

[ C ]

(x) Ni funzo gani linalotokana na Mtume Muhammad (S.A.W) kuanza kulingania Uislamu watu wa Makkah kwa siri katika miaka mitatu ya mwanzo ya utume wake?

A Muhimu kuwa wasiri mwanzo wa harakati za daa'wa
B Ili kazi ya kulingania watu ifanikiwe lazima ifanywe na mitume
C Makafiri hawawezi kukubali kuona Uislamu unakuwa
D Ili Waislamu wafanikiwe lazima kuficha mbinu za daa'wa.

[ C ]

Kielelezo 1.1 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali 1

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Amali gani inatoa nafasi kubwa kwa mtu kuwa mchamungu zaidi kwa mujibu wa Uislamu?
A Kusali katika msikiti wa Makkah
B Kufunga Sunnah katika miezi mitukufu
C Kuzama kielimu katika fani mbalimbali
D Kusimama usiku katika msikiti wa Aqsa

[ B ]

(ii) Muislamu wa kweli anaonekana na wengine katika jamii kwa ishara gani?
A Tabia na mwenendo mwema
B Majina mazuri ya kiarabu
C Mavazi na mwendo wake
D Kutumia muda mrefu msikitini

[ C ]

(iii) Ufafanuzi gani unatosheleza kutoa maana sahihi ya Nisab katika elimu ya Zaka?
A Kiwango cha juu cha mali inayostahiki kutolewa Zaka
B Kiwango cha kati cha mali inayostahiki kutolewa Zaka
C Kiwango maalumu cha mali inayostahiki kutolewa Zaka
D Kiwango cha mwisho cha mali inayostahiki kutolewa Zaka

[ B ]

(iv) Jambo gani linaashiria uzuri wa dini ya Uislamu kwa kuzingatia wepesi wa mafunzo na taratibu zake?
A Kusamehewa Sala kwa msafiri
B Kukusanya Sala kwa mgonjwa
C Kusamehewa Sala kwa mgonjwa
D Kusamehewa Sala kwa mjamzito

[ D ]

(v) Kwa nini Sala za Sunnah zimesisitizwa sana katika Uislamu?
A Zinaongeza thawabu kwa waumini
B Zinamuwezesha mtu kuwafikia Maswahaba
C Zinasababisha watu kufanana na Mitume
D Ni njia ya kufikia uchamungu kwa wepesi

[ B ]

(vi) Surat-Fat-ha inajulikana kwa majina mbalimbali **isipokuwa**
A *Faatihatul-kitaab* B *Ummul-kitaab*
C *Assab'ul-Mathaan* D *Al-Bayaana*

[ C ]

(vii) Katika usomaji wa Qur'an herufi *Nuun* yenye *Sakna* inapokutana na *Bee* (ب) yenye *Fat-ha* inasababisha kupatikana kwa hukumu gani?
A *Idghaam* B *Idghaam* yenye *ghunna*
C *Idghaam* pamoja na *ghunna* D *Idghaam Mutamaathilayn*

[ A ]

(viii) Kazi ya uchambuzi na uhakiki wa Hadithi iliyofanywa na wanazuoni sita mashuhuri ilijitokeza katika kipindi gani?
A Wakati wa Mtume (SAW)
B Wakati wa Maswahaba
C Wakati wa Tabiina
D Wakati wa Tabi'i tabiin.

[ A ]

(ix) Hadithi iliyokubaliwa na Maimamu wanne isipokuwa Bukhari na Muslim inapewa daraja gani?
A Daraja la Tatu B Daraja la Tano
C Daraja la Saba D Daraja la Nane

[ D ]

(x) Ni funzo gani linalotokana na Mtume Muhammad (S.A.W) kuanza kulingania Uislamu watu wa Makkah kwa siri katika miaka mitatu ya mwanzo ya utume wake?
A Muhimu kuwa wasiri mwanzo wa harakati za daa'wa
B Ili kazi ya kulingania watu ifanikiwe lazima ifanywe na mitume
C Makafiri hawawezi kukubali kuona Uislamu unakuwa
D Ili Waislamu wafanikiwe lazima kuficha mbinu za daa'wa.


[ B ]

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Swali la 1.

### 2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu

Swali lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu katika mada ndogo ya kusimamisha Swala. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuoanisha nguzo tano za Udhu zilizokuwa katika orodha A (i) - (v) na vitendo vinavyokamilisha nguzo hizo vilivyokuwa katika orodha B (A) – (G) kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika jedwali alilopewa. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi kuelewa utaratibu na mpangilio wa nguzo za Udhu.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 48,159 (55.04%) walipata alama 2 na 3 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 26,960 (30.81%) walipata alama 4 na 5 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, wanafunzi 12,383 (14.15%) walipata alama 0 na 1 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2.*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo asilimia 85.85 ya wanafunzi waliofanya swali hili walipata alama 3 hadi 5 ikilinganishwa na asilimia 14.15 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 na 1).

Wanafunzi waliofaulu katika swali hili; walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Nguzo za Uislamu hasa katika masharti ya Swala kipengele ambacho swali hilo liliundwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele ni kama ifuatavyo:

Kipengele cha (i); mwanafunzi alitakiwa kubaini Nguzo ya Kwanza ya Udhu, ambapo wanafunzi mahiri katika mada ya Swala walielewa vema kipengele hicho na kuoanisha kwa usahihi kwa kuchagua herufi *F Kuweka nia.* Wanafunzi hao walielewa kuwa, ili ibada ya Udhu ikamilike kama ilivyo katika ibada zingine maalum ni lazima itanguliwe na kuweka Nia. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki; baadhi yao walichagua herufi *E Kuosha uso* na wengine walichagua *C Kuosha mikono.* Majibu hayo mawili hayakuwa sahihi kwa sababu kuosha uso ni nguzo ya pili na kuosha mikono ni nguzo ya tatu katika nguzo za udhu, wanafunzi wengi walichagua herufi hizo kwa kuwa ni nguzo za kwanza za vitendo vinavyoonekana.

Kipengele cha (ii); mwanafunzi alitakiwa kubaini nguzo ya Pili ya Udhu, ambapo wanafunzi weledi katika mada ya Sala waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi *E Kuosha uso.* Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, miongoni mwao walichagua herufi C *Kuosha mikono,* na wengine walichagua kipotoshi D *Kuosha kichwa.* Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa sababu baadhi yao waliendelea kuunganisha nguzo ya tatu (*Kuosha mikono*) kwa kuwa waliacha nguzo ya kwanza (Nia) badala yake wakaanza na nguzo ya pili. Wengine waliochagua kipotoshi D *Kuosha kichwa* walionesha kukosa maarifa kuhusu nguzo za udhu kwani kitendo hicho si katika nguzo za udhu.

Kipengele cha (iii); mwanafunzi alitakiwa kubainisha Nguzo ya tatu ya Udhu, ambapo wanafunzi weledi katika mada ya Kusimamisha Sala waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi *C Kuosha mikono.* Kwa upande mwingine wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, baadhi yao walichagua herufi A *Kupaka maji kichwa* baada ya kukosa kuiweka nguzo ya kwanza (Nia) katika nafasi yake. Hiyo haikuwa sahihi kwa sababu ni nguzo ya nne ya udhu. Wengine walichagua herufi E *Kuosha uso*, ambayo ni nguzo ya pili ya udhu.

Katika kipengele cha (iv); mwanafunzi alitakiwa kuonesha Nguzo ya Nne ya Udhu, ambapo wanafunzi walioelewa vema mada ya kusimamisha

Swala waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi A *Kupaka maji kichwa.* Wanafunzi hao walielewa kuwa, kupaka maji kichwa ni nguzo ya nne katika mpangilio wa nguzo za udhu.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, baadhi yao walichagua kipotoshi D *Kuosha kichwa,* ambapo halikuwa jibu sahihi kwa sababu walishindwa kupambanua kuwa *kuosha kichwa* ni miongoni mwa Sunnah za Udhu na sio katika nguzo zake. Wanafunzi wengine walichagua herufi *G Kuosha miguu* na *B Kufuata utaratibu.* Vipengele hivyo, havikuwa jibu sahihi kwa kuwa kuosha miguu ni nguzo ya tano ya Udhu na kufuata utaratibu ni nguzo yake ya sita ambapo swali lake halikuulizwa.

Kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kuoanisha Nguzo ya Tano ya Udhu na kitendo kinachokamilisha nguzo hiyo. Wanafunzi weledi katika mada ya kusimamisha Sala waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi G *Kuosha miguu,* wanafunzi hao walielewa vyema mpangilio wa nguzo za Udhu hivyo waliweza kutambua jibu sahihi. Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua herufi *B Kufuata utaratibu* ambalo sio jibu sahihi, kwa sababu ni nguzo ya sita ya Udhu na haikuulizwa kwenye orodha A ya maswali. Wengine walichagua herufi F *Kuweka nia,* ambalo halikuwa jibu sahihi kwa kuwa ni nguzo ya kwanza katika mpangilio wa nguzo za Udhu. Aidha, sampuli ya majibu sahihi na yasiyo sahihi ya wanafunzi katika swali hili yameoneshwa katika kielelezo Na. 2.1 na 2.2. mutawalia.

2. Oanisha nguzo tano za Udhu katika **Orodha A** na vitendo vinavyokamilisha nguzo hizo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu katika sehemu ya kuandika majibu uliyopewa.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Nguzo ya Kwanza | A Kupaka maji kichwa |
| (ii) Nguzo ya Pili | B Kufuata utaratibu |
| (iii) Nguzo ya Tatu | C Kuosha mikono |
| (iv) Nguzo ya Nne | D Kuosha kichwa |
| (v) Nguzo ya Tano | E Kuosha uso |
| | F Kuweka nia |
| | G Kuosha miguu |

**Majibu**

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | F | E | C | A | G |

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

2. Oanisha nguzo tano za Udhu katika **Orodha A** na vitendo vinavyokamilisha nguzo hizo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu katika sehemu ya kuandika majibu uliyopewa.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Nguzo ya Kwanza | A Kupaka maji kichwa |
| (ii) Nguzo ya Pili | B Kufuata utaratibu |
| (iii) Nguzo ya Tatu | C Kuosha mikono |
| (iv) Nguzo ya Nne | D . Kuosha kichwa |
| (v) Nguzo ya Tano | E Kuosha uso |
| | F Kuweka nia |
| | G Kuosha miguu |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | B | C | D | E | F |

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 2


## 2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi (3, 4, 5, 6, 7, 8 na 9). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote. Maswali hayo yaliandaliwa kutoka katika mada za *Kumjua Mwenyezi Mungu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Mambo ya lazima kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Sunnah na Hadithi, Historia katika Uislamu* na *Bara Arab Zama za Jahiliyyah karne ya 6 A.D.*

### 2.2.1 Swali la 3: Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W)

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Njia za Kumjua Mwenyezi Mungu,* ambapo mwanafunzi alitakiwa kutumia hoja nne kubainisha udhaifu wa *Fitrah* na vipaji vya kiakili katika kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua udhaifu wa njia hizo zinapotumika kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W).

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 87,502 (100%) walifanya swali hili. Miongoni mwao wanafunzi 65,572 (74.90%) walipata sufuri 0. Wanafunzi 81,820 (93.51%) walipata 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Aidha, wanafunzi 5,117 (5.84%) walipata alama 2.5 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 565 (0.65%) pekee walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3.*

Chati Na. 3 inaonesha hali ya ufaulu dhaifu katika swali hili kwakuwa asilimia 93.51 ya wanafunzi walipata alama za chini (0 hadi 2) ikilinganishwa na asilimia 6.43 ya wanafunzi waliofaulu.


Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, wanafunzi walipata ufaulu wa chini katika swali hili kwakuwa walikosa maarifa kuhusu njia za kumjua Mwenyezi Mungu (S.W). Baadhi yao walitoa hoja ambazo hazikuwa na mantiki kama vile: *Pindi mwanadamu anapougua Fitrah na vipaji vitaugua na pia atapoteza kumbukumbu, sio wanadamu wote waliotambua vipaji vyao, sio rahisi kwa wanadamu kutambua kuwa vipaji vya mwanadamu ni njia ya kumjua Allah (S.W)*. Hoja hizi zinaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa juu ya dhana ya Fitrah wala vipaji vya kiakili.

Kadhalika, wanafunzi wengine walitaja ishara mbalimbali za Fitrah pasipo kujua kwani hazikuwa na muungano na mukhtadha wa swali, mwanafunzi mmoja aliandika: *Fitrah ya mwanadamu ni kumuabuadu, Fitrah ya udhaifu wa mwanadamu ni kuamini Mungu yupo, Sio rahisi kwa wanadamu kutambua kuwa vipaji vya mwanadamu ni njia ya kumjua Allah*. Majibu haya yanaonesha kuwa mwanafunzi hakuwa na maarifa kuhusu udhaifu wa Fitrah na vipaji vya kiakili. Mwingine alijibu: *Kutumia maarifa yake ili kufanya mambo kwa ufanisi, kushushiwa Qur'an na Mwenyezi Mungu*

*(S.W).* hoja ambazo ziliashiria kueleza sifa ya Mitume (A.S) na sio udhaifu wa *Fitrah* na vipaji vya akili.

Kundi lingine katika wanafunzi waliopata alama za chini katika swali hili, walishindwa kubaini matakwa ya swali husika. Miongoni mwao walichanganya Nguzo za Imani na kuainisha nguzo hizo kama vile: *Kuamini Malaika, Kuwepo kwa Siku ya mwisho, Kuamini kadari zake.* Majibu hayo yalitaja baadhi ya Nguzo za Imani ya Kiislamu badala ya kuainisha udhaifu wa Fitrah na vipaji vya kiakili. na kuashiria kuwa wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali.

Mwanafunzi mmoja aliandika*: Mwenye kusoma, Mwenye kusimamisha na mwenye kusoma Qur'an kila wakati*, *Wenye kutimiza vigezo vyote, Anatakiwa awe amefikisha umri unaohitajika na awe ana kila sifa ya Mitume.* Majibu hayo yaliashiria kueleza sifa za muumini badala ya udhaifu wa Fitrah na vipaji vya akili. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


3. **Kwa kutumia hoja nne, bainisha udhaifu wa Fitrah na vipaji vya kiakili katika kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W).**

(i) Kutokua na Akili timamu.

(ii) Walemavu wa kuona, kusikia na kuongea.

(iii) Waliokua na Akili timamu


(iv) Walioangamia

Kielelezo Na. 3.1 Sampuli Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.1 mwanafunzi ameorodhesha sifa zinazoashiria makundi mbalimbali ya watu ambayo hayana uhusiano na dhana ya Fitrah na vipaji vya mwanadamu. Majibu hayo yanaonesha kuwa mwanafunzi alikosa maarifa katika mada ya Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W).

Wanafunzi wachache waliofaulu (6.43%) katika swali hili walionesha kuwa na maarifa kuhusu njia za kumjua Mwenyezi Mungu (S.W) na walielewa vema matakwa ya swali. Wanafunzi hao waliweza kubainisha udhaifu wa Fitrah na Vipaji vya kiakili katika kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa hoja sahihi kama vile; *(i)Binadamu anathiriwa na mazingira anayoishi, (ii) Viungo vya binadamu vina udhaifu,*

*(iii) Binadamu anaathiriwa sana na ubinafsi na uchoyo, (iv) Sayansi anayoitumia mwanadamu ina udhaifu.* Kielelezo Na.3.2 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.



3. **Kwa kutumia hoja nne, bainisha udhaifu wa Fitrah na vipaji vya kiakili katika kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W).**

(i) Maumbile ya mwanadamu huathiriwa kwa kiasi kikubwa na mazingira.

(ii) Mwanadamu hawezi kutumia vipaji vyake ipasavyo kulingana na mapungufu aliyokuwa nayo.

(iii) Binadamu huathiriwa na ubinafsi na uchoyo aliokuwa nao.

(iv) Mwanadamu hawezi kutenda jambo lolote bila kutaka msaada kwa Allah (S.w).


Kielelezo Na. 3.2 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 3

### 2.2.2 Swali la 4: Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) kutoka katika mada ya Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, mada ndogo ya Haja ya Dini kwa Mwanadamu. swali lilipima umahiri wa wanafunzi kuchambua dhana ya Dini kwa mazingatio ambayo mwanadamu anapaswa kuishi nayo kutoka katika Qur'an.

Katika kipengele cha 4 (a); mwanafunzi alitakiwa kubainisha dhana ya Dini kwa muktadha wa aya ya (3:83) ambapo Mwenyezi Mungu amesema: *''Jee (watu) wanataka Dini isiyokuwa ya Allah na hali kila kilichopo mbinguni na ardhini kimejisalimisha kwake kipende kisipende. Na kwake watarejeshwa wote''.* Aidha, katika kipengele cha 4(b) mwanafunzi alitakiwa kutoa mafunzo matatu yanayopatikana kutokana na tafsiri ya aya hiyo.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 87,502 (100%) walifanya swali hili. Kati yao 44,530 (50.89%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu dhaifu na wanafunzi 35,211 (40.24%) walipata alama za 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Aidha, wanafunzi 7,761 (8.87%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 4 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4.*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 50.89 ya wanafunzi walipata alama za chini (0 hadi 2.5). ikilinganishwa na asilimia 49.11 ya wanafunzi waliofaulu kwa alama kati ya 3 hadi 10.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, wanafunzi waliopata ufaulu hafifu katika swali hili; baadhi yao hawakuwa na maarifa kuhusu Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Katika kipengele cha 4(a) ambacho wanafunzi walitakiwa kubainisha dhana ya Dini kwa muktadha wa Aya waliyopewa, baadhi ya wanafunzi hao walijibu kwa maelezo kama vile; *Dini ni kitendo cha kumuabudu Allah (S.W) na kufuata maamrisho yake.* Tafsiri ambayo ni kinyume na mtazamo wa Qur'an. Baadhi walichanganya maana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu na maana ya Dini ya Kiislamu. Mwanafunzi mmoja aliandika kama ifuatavyo; *Dini ni utaratibu na sheria zote zilizowekwa na Mwenyezi Mungu ili kuzifuata kwa unyenyekevu.* Wengine walichanganya dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu na umuhimu wa Dini, mmoja kati ya wanafunzi hao aliandika; *Dini inatusaidia kujua ya kwamba sisi sote tumeumbwa na Allah kwa hiyo kila mmoja anapaswa kufuata jinsi ya Allah anavyotaka.* Kwa ujumla maelezo waliyoyatoa wanafunzi hao yalionesha

kushindwa kuelewa swali kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mtazamo wa Uislamu juu ya Dini.

Wanafunzi wengine waliandika hoja mbali mbali kama vile; *Dhana ya dini ni Qur'an na hadithi za Mtume (S.A.W).* Mwingine aliandika; *Dini ni kuwa na yakini moyoni*. Mwingine aliandika; *Dini ni kumjua Allah, Mtume (S.A.W) katika kipindi chote cha Utume wake,* isitoshe mwanafunzi mmoja alieleza kuwa*; Dini ni kile kilichoumbwa kwa uwezo wa Allah kitarudishwa kwake na viumbe hai watarudi kwa udongo na vitu vyengine.* Hoja zote hizi zilionesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Dini katika Uislamu. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi

4. "Je, (watu) wanataka Dini isiyokuwa ya Allah na hali kila kilichopo mbinguni na ardhini kimejisalimisha kwake kipende kisipende. Na kwake watarejeshwa wote." Qur'an (3:83).

(a) Bainisha dhana ya Dini kwa muktadha wa Aya hiyo.
kusamehewa Sala kwa msafiri.........................................

Kielelezo Na. 4.1 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Swali la 4 (a)

Katika kielelezo Na. 4.1 mwanafunzi alionesha kukosa maarifa kuhusu dhana ya Dini hivyo alinukuu hoja kutoka katika vipotoshi vya swali la 1 iv(A) ambacho hakina uhusiano wowote na swali lililoulizwa.

Katika kipengele cha 4(b); wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walitoa hoja mbalimbali zisizoendana na matakwa ya swali kwa sababu ya kukosa maarifa. Baadhi ya wanafunzi walitoa tafsiri ya Suratul Fat-ha na kuchanganya na mafunzo yanayopatikana kutokana na tafsiri ya aya waliyopewa kama vile: *(i) Shukraan njema zinastahiki kusifiwa Mwenyezi Mungu (ii) Hakika ni mwingi wa rehma na mwenye kurehemu*. Mwingine aliandika tafsiri ya Suratul Ikhlaas; *(i) Mwenyezi Mungu ni mmoja (ii) Hakuzaa wala hakuzaliwa (iii) Hakufanana na yeyote*. Mwingine alitaja aina za dini; *(i) Dini za watu, (ii) Dini ya kikafiri, (iii) Dini ya kiislamu.* Pamoja na kuchanganya dhana mbalimbali katika kujibu swali hili, wanafunzi hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aya waliyopewa.

Kadhalika, wanafunzi wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi walitoa hoja mbalimbali kama vile; *(i) Mfumo wa maisha ya mwanadamu. (ii)*

*Huweza kusaidia kutenganisha makundi mbali mbali ya watu. (iii) Huweza kusaidia kujua maana sahihi ya dini.* Mwanafunzi mmoja alieleza*: (i) Nimejifunza kuwa watu wanataka vitu vya Allah (S.W) hali ya kuwa Allah hawamtaki (ii) Watu wanataka kuishi kwa uhuru pasipo kumjua Mwenyezi Mungu. (iii) Kuswalia masanamu (mzimu) na kwenda katika dini isiyo ya haki.* Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu mada ya Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele 4(b).

(b) Toa mafunzo matatu yanayopatika kutokana na tafsiri ya aya hiyo.

(i) Kufuza elimu kulawa sana kwa sababushi

(ii) zina sababisha watu kufana na mitume

(iii) Ni njia ya kufikia uchamungu kwa wepesi

Kielelezo Na. 4.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 4 (b)

Katika kielelezo Na. 4.2 mwanafunzi alishindwa kabisa kutoa mafunzo yanayotokana na tafsiri ya aya aliyopewa badala yake alinukuu baadhi ya vipotoshi katika swali la 1 (v).

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wanafunzi waliofaulu katika swali hili walielewa vema matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an. Hivyo waliweza kutumia maarifa yao vizuri na kujibu swali hilo kwa usahihi kama vile: *Dini ni jumla ya mambo yote anayoyafanya na kuyatenda mwanadamu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kila siku ya kijamii na kibinafsi.* Kielelezo Na. 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi aliyefaulu.


4. "Je, (watu) wanataka Dini isiyokuwa ya Allah na hali kila kilichopo mbinguni na ardhini kimejisalimisha kwake kipende kisipende. Na kwake watarejeshwa wote." Qur'an (3:83).

(a) Bainisha dhana ya Dini kwa muktadha wa Aya hiyo.

Dini: Ni mfumo wa maisha anaoufuata mwanadamu katika kukiendea kipengele cha maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na kijamii. Hivyo, aya hii inatuonesha kuwa ni muhimu kwa wanadamu kufuata Dini ya Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha yak

Kielelezo 4.3 Sampuli ya Majibu Sahihi Swali la 4 (a)

Aidha, katika kujibu kipengele cha 4 (b), wanafunzi hao walibainisha mafunzo yanayopatikana katika aya waliyopewa kama ifuatavyo*; (i) Allah (S.W) ndiye mlezi mkuu na mmiliki wa wanadamu na kila kitu. (ii) Ni muhimu kila mtu kutenda mema na kuacha maovu kwani atarejeshwa kwa Mola wake na (iii) Hatunabudi kufuata mwongozo wa Dini kwa mazingatio kwani, dini inamtakasa mtu na aina zote za dhulma na utumwa.* Kielelezo Na. 4.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefaulu.


(b) Toa mafunzo matatu yanayopatika kutokana na tafsiri ya aya hiyo.

(i) Tunajifunza kuwa ~~chanzo cha~~ dini ya Allah (S.W) ndiyo dini sahihi na inayopaswa kufuatwa na watu katika jamii

(ii) Vitu vyote vilivyopo mbinguni na Ardhini vinamtegemea Allah na vinajinusuru kwa kujisalimisha kwa Allah (S.W).


(iii) Watu vitu vyote vilivyo duniani vyote vitarejeshwa kwa Muumba ambaye ni Allah ~~S.A~~ (S.W) ambaye yeye kwake halishindikani lolote katika jambo.

Kielelezo Na. 4.4 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 4 (b)

### 2.2.3 Swali la 5: Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu* katika mada ndogo ya *Kumsalia Maiti*. Swali lilikuwa na vipengele viwili 5(a) na 5(b) ambapo katika kipengele 5(a) mwanafunzi alitakiwa kubainisha masharti matatu ya Swala ya maiti, wakati 5(b) mwanafunzi alitakiwa kubainisha mambo mawili ya Sunnah yanayofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya sala ya Maiti. Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi kutekeleza ibada ya Sala ya maiti.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 47,723 (54.54%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 36,620 (41.85%) walipata alama 2.5 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 3,159 (3.61%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 5.





**Chati Na. 5:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5.*

Chati Na. 5. inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 54.54 ya wanafunzi walipata alama za chini (0 hadi 2.5) ikilinganishwa na asilimia 49.11 ya wanafunzi waliofaulu kwa alama kati ya 3 hadi 10.

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa kuhusu Sala ya Maiti. Miongoni mwa ambao hawakuelewa vema matakwa ya swali katika kipengele cha 5(a) walitaja Nguzo za Sala ya Maiti badala ya masharti ya Sala ya Maiti kama vile*: (i) Kuwa na nia moyoni, (ii) Kumuombea dua maiti.* Wengine walichanganya taratibu za kumuosha maiti na masharti ya Sala ya maiti kama vile; (i) *Hutakiwi kumsema wakati wa kumuosha (ii) Unatakiwa kumgeuza upande mmoja mmoja, (iii) Kuchukulishwa udhu Maiti.* Mwingine alitaja masharti ya Sala ya Ijumaa badala ya masharti ya Sala ya maiti kama vile; *(i) Waswali wenyeji wa mji tu. (ii) Iswaliwe na wanaume tu*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuelewa vema matakwa ya swali.

Kundi lingine katika waliopata ufaulu hafifu walishindwa kabisa kutoa hoja zinazojibu swali. Mmoja kati ya wanafunzi hao alinukuu maswali kutoka katika swali husika na baadhi ya vipengele vya maswali mengine. Mwanafunzi huyo aliandika: (i) *Ni mambo gani mawili ya Sunnah*

*yanayofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya sala ya Maiti (ii) Vipaji vya kiakili katika kuthibiotisha kuwepo, (ii) Masharti matatu ya Sala ya Maiti ya kwanza.* Kadhalika, mwingine aliandika; *Huswaliwa rakaa zaidi ya nne.* Majibu ya wanafunzi hao yaliashiria kukosa maarifa kuhusu sala ya maiti hivyo walibuni majibu yasiyokuwa na mantiki. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5(a).


5. (a) Bainisha masharti matatu ya Sala ya maiti?

(i) ~~Aogeshwa~~ kutia nia

(ii) ~~kusom~~ Takbila ya kuhitimia

(iii) kusoma Surat Fatha

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 5(a)

Katika kipengele cha 5(b) ambapo mwanafunzi alitakiwa kubainisha mambo mawili ya Sunnah yanayofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya Sala ya maiti, baadhi ya wanafunzi walichanganya mambo mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi. Mwanafunzi mmoja alichanganya Sunnah zinazofanyika kabla ya takbira ya kwanza na nguzo za Sala kwa kuandika: *(i) Kutia nia, (ii) Kutoa salamu.* Na mwingine alitaja mambo ya lazima anayofanyiwa maiti wa Kiislamu kama vile; *(i) Kumuosha Maiti, (ii) Kumvika sanda.* Pia wapo waliobainisha Sunnah za kumuosha Maiti kama vile; *(i) Kama Maiti ya kike ikioshwa na mume wake ni Sunnah, (ii) Kupigishwa mswaki Maiti ni Sunnah, (iii) Kumkata kucha maiti ni Sunnah.* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali.

Wanafunzi waliokosa maarifa kuhusu Sunnah kabla ya takbira ya kwanza ya Sala ya maiti walitoa majibu kama vile; *(i) Kunasababisha mtu kufanana na mitume, (ii) Kinamuwezesha mtu kuwafikia Maswahaba.* Mwingine aliandika nguzo ya kwanza ya Uislamu yaani: *Kutamka shahada mbili.* Majibu ya wanafunzi hawa yalionesha wazi kuwa walikosa maarifa kuhusu Sunnah za Sala ya maiti. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuelewa Sunnah za swala ya Maiti kabla ya takbira ya kwanza.

(b) Ni mambo gani mawili ya Sunna yanayofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya Sala ya maiti?

(i) Nia.

(ii) ~~Sulatat fadih~~ Surat-fat-ha.

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 5 (b)

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, waliopata alama za juu katika swali hili, walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sala ya maiti na walielewa vema matakwa ya swali. Katika kipengele cha 5(a) wanafunzi hao walibainisha kwa usahihi masharti ya Sala ya maiti na katika kipengele cha 5(b) waliweza kubainisha Sunnah zinazofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya Sala ya Maiti. Katika kipengele cha 5(a), wanafunzi hao waliainisha kwa ufasaha masharti ya Sala ya Maiti kama vile: (i) *Maiti anatakiwa awe Muislamu, (ii) Maiti anatakiwa asiwe shahidi na (iii) Maiti anatakiwa awe ameoshwa na kukafiniwa, (iv) Maiti awekwe mbele ya wanaomsalia.* Kielelezo Na. 5.3 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5(a).

5. (a) Bainisha masharti matatu ya Sala ya maiti?


(i) Maiti anatakiwa awe muislamu ili maiti aweze kuswaliwa lazima awe ni muislamu aliyetamka shahada.

(ii) Maiti anatakiwa asiwe shahidi maiti aliyekufa vitani akipigania katika njia ya Allah haruhusiwi kuswaliwa na wala kuoshwa.

(iii) Maiti anatakiwa awe ameoshwa na kukafiniwa ili maiti aweze kuwa na swala sahihi lazima awe maiti ameoshwa na pia amevishwa sanda.

Kielelezo Na. 5.3: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 5(a)

Aidha, katika kipengele cha 5(b) wanafunzi hao waliweza kubainisha mambo ya Sunnah yanayofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya Sala ya maiti kama vile; (i) *Imamu kukaa usawa wa mabega kama Maiti ni wa kiume na kukaa katikati kama Maiti ni wa kike na (ii) Maamuma waliopo nyuma ya imamu kukaa katika safu za witri, (iii) Kutangaza na kumtakasa na madeni.* Kielelezo Na. 5.4 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5(b).



(b) Ni mambo gani mawili ya Sunna yanayofanyika kabla ya takbira ya kwanza ya Sala ya maiti?

(i) Imamu kukaa usawa wa mabega ya maiti kama maiti ni wakiume na kukaa katikati kama maiti ni wakike.


(ii) Maamuma walipo nyuma ya imamu kukaa katika safu za witiri witiri ni kuanzia 3,5,7,9,11,13.

Kielelezo Na. 5.4: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 5(b).

### 2.2.4 Swali la 6: Qur'an

Swali hili lilitoka katika mada ya Qur'an mada ndogo ya Aina za Wahyi. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuainisha njia tano anazozitumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake. Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua njia mbalimbali za *wahyi* (anazotumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake).


Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 57,577 (65.80%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Wanafunzi 17,770 (20.31%) walipata alama 2.5 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 12,155 (13.89%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi Katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 86.11 ya wanafunzi hao walipata alama 2.5 hadi 10 ikilinganishwa na asilimia 13.89 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 hadi 2).

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wanafunzi waliofaulu katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia za mawasiliano kati ya Allah (S.W) na waja wake na walielewa vema matakwa ya swali. Wanafunzi hao waliainisha kwa ufasaha njia anazozitumia Allah (S.W) katika kuwasiliana na waja wake kama vile; *(i) Njia ya ndoto za Kweli, (ii) Njia ya Ilhamu, (iii) Njia ya Maandishi, (iv) Njia ya kuletewa Malaika na (v) Njia ya Wahyi*. Kielelezo Na. 6.1 Kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 6.



6. Mwenyezi Mungu (S.W) anawasiliana na waja wake katika zama mbalimbali hapa duniani ili kuwapa mwongozo wa maisha kwa ajili ya kutimiza lengo kuu la kuumbwa kwao. Ainisha njia tano anazozitumia katika mawasiliano hayo.

(i) Il-hamu. Hii ni njia inayopenyeka bila ya mtu kujijua.
(ii) Nyuma ya pazia. Hichi ni kitendo cha kuzungumza kupitia sauti
(iii) Kutumwa malaika. Kama alivyotumwa malaika Jibril (a.s)
(iv) Njia ya ndoto. Kila ndoto waliyokuwa wakiota mitume ni za kweli
(v) Njia ya maandishi. Mbao zilizoandikwa kwa tayari.

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 6.

Kwa upande mwingine; wanafunzi waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao walionesha kutoelewa matakwa ya swali, hali iliyosababisha wanafunzi hao kuandika hoja tofauti na mahitaji ya swali. Wengine walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu njia anazotumia Allah (S.W) kuwasiliana na waja wake.

Baadhi ya wanafunzi walinukuu majina ya Qur’an kama vile: (i) *Faatihatul- kitaab,* (ii) *Ummul kitaab,* (iii) *Al- Bayaana* (iii) *Assab ‘ul-Mathaan*. Na wengine waliandika majina ambayo hayakuwa na mfuatano unaoeleweka, kama vile; *(i) Uislamu (ii) Malaika, (iii) Utumwa, (ii) Ugonjwa (iv) mjamzito*. Wengine walioandika ibada mbalimbali maalumu, kama vile*; (i) Funga za Sunnah na mwezi mtukufu wa Ramadhani, (ii) Swala (iii) Sadaka na Zaka*. Majibu hayo yalionesha kuwa wanafunzi walikosa maarifa ya kutosha juu ya mada ya njia za mawasiliano ya Allah kwa waja wake.

Wanafunzi wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali husika, hivyo walichanganya njia anazotumia mwanadamu kumjua Mwenyezi Mungu na njia anazotumia Allah kuwasiliana na waja wake kama vile; *(i) Nafasi ya Fitrah (ii) Nafasi ya vipaji vya akili ya mwanadamu, (iii) Nafasi ya nafsi ya mwanadamu, (iv) Nafasi ya Wahyi*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walishindwa kubaini matakwa ya swali husika. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

6. Mwenyezi Mungu (S.W) anawasiliana na waja wake katika zama mbalimbali hapa duniani ili kuwapa mwongozo wa maisha kwa ajili ya kutimiza lengo kuu la kuumbwa kwao. Ainisha njia tano anazozitumia katika mawasiliano hayo.

(i) kuSamehewa Sala Kwa msafiri
(ii) Kukusanya Sala Kwa mgonjwa
(iii) KuSamehewa Sala kwa mgonjwa
(iv) Kusamehewa Sala Kwa mjamzito
(v) Ainisha njia tano anazozitumio katiku mawasiliana hay

Kielelezo Na 6.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6.

Katika kielelezo Na. 6.2 mwanafunzi alinukuu swali na vipotoshi katika swali la 1 (iv) badala ya kubainisha njia za mawasiliano anazotumia Mwenyezi Mungu kwa waja wake.

### 2.2.5 Swali la 7: Sunna na Hadithi


Swali hili lilitoka katika mada ya Sunnah na Hadithi katika mada ndogo ya Uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W). Mwanafunzi alitakiwa kusoma Hadithi aliyopewa kisha kujibu maswali yake katika vipengele (a), (b) na (c); Hadithi aliyopewa mwanafunzi katika swali hilo ilikuwa;

Abuu Hurayrah (R.A) amesimulia kuwa Mtume (S.A.W) amesema: ‘’Allah (S.W) amesema: *‘’hakika Mimi ni mwingi wa kujitosheleza kiasi kwamba sihitaji mshirika yoyote…”* (Muslim na Ibnu Majah).

Katika kipengele cha 7(a) (i) mwanafunzi alitakiwa kubainisha aina ya Hadithi hiyo kwa kuzingatia sifa zake, na kipengele cha 7(a) (ii) mwanafunzi alitakiwa kutoa sababu kuthibitisha aina ya Hadithi aliyotaja katika kipengele (a) (i). Aidha, katika kipengele 7(b) mwanafunzi alitakiwa kutoa tofauti tatu za aina kuu za Hadithi kwa kuzingatia sifa.

Vile vile katika kipengele cha 7 (c) mwanafunzi alitakiwa kutoa tofauti iliyopo kati ya Hadithi aliyopewa katika 7 (a) (i) na Hadithi Nabawiy. Kwa ujumla swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kuchambua Hadithi za Mtume (S.A.W).

Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wanafunzi 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu, wanafunzi 72,492 (82.85%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 12,261 (14.01%) walipata alama 2.5 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 2,749 (3.14%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, kati ya wanafunzi waliokuwa na ufaulu dhaifu, wanafunzi 53,216 (60.80%) walipata 0. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 7.*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani asilimia 82.85 ya wanafunzi walipata alama 0 hadi 2 ikilinganishwa na asilimia 17.15 ya wanafunzi waliofaulu.

Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu wa chini katika swali hilo ulisababishwa na wanafunzi kukosa maarifa kuhusu Sunnah na Hadithi na wengine kushindwa kubaini matakwa ya swali katika vipengele vyote. Katika kipengele cha 7(a)(i); baadhi ya wanafunzi hao walinukuu jina la msimulizi; *Abuu Hurayrah.* Wengine waliandika*; Hadithi sahihi,* na

mwingine alijibu *Hadithi ya Mtume (S.A.W).* Majibu ya wanafunzi hao yaliashiria kuwa walikosa maarifa kuhusu aina kuu za Hadithi.

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili, walionesha kushindwa kubaini matakwa ya swali hivyo, walichanganya na aina za Tawhiid, nao waliandika; *Hadithi Rubbubiyyah.* Mwingine alichanganya na dhana ya Ihsan ambapo aliandika; *Enyi Waumini muaminini Mwenyezi Mungu kama kwamba munamuona.* Licha ya kuwa majibu hayo hayakuendana na hitajio la swali lakini pia yaliashiria kukosa maarifa juu ya Sayansi ya Hadithi kwa ujumla. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 7 (a) (i).

7. (a) Soma Hadithi ya Mtume (S.A.W) uliyopewa kisha jibu maswali katika vipengele (i) hadi (ii).

Abuu Hurayrah (R.A) amesimulia kuwa Mtume (S.A.W) amesema: *"Allah (S.W) amesema: "Hakika Mimi ni mwingi wa kujitosheleza kiasi kwamba sihitaji mshirika yoyote..."* (Muslim na Ibnu Majah).

(i) Bainisha aina ya hadithi kwa kuzingatia sifa katika hadithi uliyopewa.

Hakika mimi ni mwenye ~~wa~~nguvu na kujitosheleza akika hakuna mwingine wa zaidi yangu.

Kielelezo Na. 7.1 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Kipengele cha 7(a)

Katika kipengele cha 7(a)(ii) ambacho wanafunzi walitakiwa kuthibitisha aina ya Hadithi iliyotajwa katika kipengele 7(a) (i), baadhi yao walioshindwa kujibu kwa usahihi kwakutoa hoja kama vile; *Hadithi ina maadili juu ya Uislamu,* mwingine aliandika*; Kwa sababu hadithi nyingine zilikuwa za uongo.* Wengine walinukuu rawi wa Hadithi yani*; Muslim na Ibnu Majaah,* na mwingine alijibu*; Kwa sababu Hadithi ina waandishi wake na haipingi hadithi za Mitume wengine,* na wapo waliojibu*; Dini ni mafunzo kwa watu wote.* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu sayansi ya Hadithi kwa ujumla. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 7 (a) (ii)


(ii) Toa sababu kuthibitisha aina ya hadithi iliyotajwa katika (a) (i).

watu kwa sababu dini ya uslimu katika mung mbingu pao

Kielelezo Na. 7.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Kipengele cha 7(a) (ii).

Katika kipengele cha 7(b); wanafunzi waliopata ufaulu wa chini, baadhi yao walibuni majibu ambayo sio matakwa ya swali, baadhi yao waliandika: *Utawa*, *Faradhi, Imemalizia na jina Muslim.* Na wengine walijibu*; Kufuatilia manabii, Kuelimisha, Kukubaliana na manabii wa Allah.* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu tofauti baina ya aina kuu za Hadithi kwa kuzingatia kigezo cha sifa.

Wanafunzi wengine katika waliopata ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo baadhi walichanganya aina kuu za Hadithi na tanzu za Hadithi kwa kigezo cha usahihi, wanafunzi hao waliandika; *Hadithi sahihi* na *Hadithi Hassan.* Wengine waliandika vipindi katika historia ya uandishi Hadithi za Mtume (S.A.W) badala ya aina kuu za Hadithi kama vile; *Kipindi cha Mtume (S.A.W), Kipindi cha Maswahaba na kipindi cha Tabiina.* Maelezo hayo yalionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 7.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 7(b).


(b) Toa tofauti tatu za aina kuu za hadithi kwa kuzingatia sifa.

(i) waislamu mbingu kuwa kuliongazia watu hafu kuwa kuona shangaa kuu zinosababishu

(ii) Sunneh kusamehe kuwa safo watu kusaidia buibui umepata kuona Alikuwasairi watu

(iii) Aina kuu hadithi kuwa safi kuu mkitano maelezo watu dhimu kuwa kuu zimoa

Kielelezo Na. 7.3 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Kipengele cha 7(b).

Mwisho, katika kipengele cha 7(c) ambacho mwanafunzi alitakiwa kubainisha namna Hadithi iliyotajwa (a) (i) (Qudusy) inavyotofautiana na Hadithi Nabawiy, ambapo wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili walitoa hoja kama vile; *(i) Kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, (ii) Na kuamini kwamba Siku ya Kiama ipo, (iii) Hadithi Nabawiyyi inazungumzia Manabii ila hadithi tajwa hapo haina uhusiano huo. (iv) Hadithi iliyotajwa hapo inataja na kutukuza sifa za Allah (S.W).* Wanafunzi hawa walionesha wazi kuwa walikosa maarifa kuhusu aina kuu za Hadithi na tofauti zake. Kielelezo Na. 7.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 7(c).

(c) Hadithi iliyotajwa katika (a) (i) inatofautianaje na hadithi Nabawiy?

(i) ~~Hak~~ Hahawu Katika na Nabawiy utunga utunga kwa chambi tatu kwa lut:

(ii) Toa sababu kuthiobitisha ~~an~~ aina ya hadithi iliyotajwa katika:

(iii) Toa tofauti tatu za aina kuu za hadithi kwa kuzingatia Sifa

Kielelezo Na. 7.4 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Kipengele cha 7(c).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi wachache (17.15%) waliofaulu katika swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sayansi ya Hadithi na walielewa vema matakwa ya kila kipengele. Aidha, katika kipengele cha 7 (a) (i) wanafunzi hao waliweza kubainisha aina ya Hadithi waliyopewa kwa usahihi na kuitaja kuwa ni; *Hadithi Qudusy*. Kielelezo Na. 7.5 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 7 (a) (i).

7. (a) Soma Hadithi ya Mtume (S.A.W) uliyopewa kisha jibu maswali katika vipengele (i) hadi (ii).

Abuu Hurayrah (R.A) amesimulia kuwa Mtume (S.A.W) amesema: "*Allah (S.W) amesema: "Hakika Mimi ni mwingi wa kujitosheleza kiasi kwamba sihitaji mshirika yoyote…*" (Muslim na Ibnu Majah).

(i) Bainisha aina ya hadithi kwa kuzingatia sifa katika hadithi uliyopewa.

Ni hadithi Qudusiy.

Kielelezo Na. 7.5 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Kipengele cha 7(a).

Aidha, katika kipengele cha 7 (a) (ii) wanafunzi hao waliweza kuthibitisha aina ya Hadithi iliyotajwa kwenye 7(a)(i) kuwa ni *Qudusy* kwa hoja kuwa; *Hadithi hiyo imeanza kwa maneno Mtume (S.A.W) amesema; "Allah amesema''*… kama mbavyo kielelezo Na.7.6 kinaonesha.


(ii) Toa sababu kuthibitisha aina ya hadithi iliyotajwa katika (a) (i).

~~Haijapingana na aya za Qur-an.~~

Imeanza kwa Mtume kusema "Allah Amesema…."

Kielelezo Na. 7.6: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Kipengele cha 7(a) (ii).

Katika kipengele cha 7(b); wanafunzi waliofaulu waliweza kuonesha kwa ufasaha tofauti baina ya aina kuu za Hadithi kwa kuzingatia sifa kama vile; (i) *Hadithi Qudusy ni habari aliyoitoa Mtume (S.A.W) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (S.W) ambayo ipo nje ya Qur'an lakini Hadithi Nabawiy ni habari aliyoitoa Mtume (S.A.W) kwa maneno yake, (ii)Hadithi Qudusy huanza na kauli ya ''Amesema Mtume; Allah amesema'' lakini Hadithi Nabawiy huanza na kauli ya ''Amesema Mtume'' (iii) Hadithi Qudusy ni chache kwa idadi yake lakini Hadithi Nabawiy ni nyingi kwa idadi.* Kielelezo Na.7.7 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 7 (b).


(b) Toa tofauti tatu za aina kuu za hadithi kwa kuzingatia sifa.


(i) Hadithi Qudusy huanza kwa mtume akisema "Allah amesema..." ila Nabawy huanza kwa maneno ya mtume

(ii) Hadithi Qudusy mtume hueleza kama Allah (s.w) aliyomshushia Hadithi Nabawi Mtume hueleza kwa maneno yake.

(iii) Hadithi Nabawy ni maneno ya mtume ila Hadithi Qudusy ni maneno ya Allah (s.w).

Kielelezo Na. 7.7: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Kipengele cha 7(b)

Kadhalika, katika kipengele cha 7(c); wanafunzi waliofaulu waliweza kuonesha kwa ufasaha tofauti iliyopo katika Hadithi iliyotajwa (a) (i) na Hadithi Nabawiy kama inavyoonekana; *(i) Hadithi Qudusy ni ile ambayo Mtume (S.A.W) ameleza na kuanza kwa kusema "Allah amesema..'' lakini Hadithi Nabawiy amesimulia Mtume bila ya kuanza kwa kusema ''Allah amesema'' (ii) Qudusy ni maneno ya Allah yaliyo nje ya Qur'an lakini Hadithi Nabawiy ni maneno ya Mtume (S.A.W) mwenyewe (iii) Hadithi Qudusy ni kidogo lakini Hadithi Nabawiy ni nyingi.* Kielelezo Na 7.8 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele hicho.


(c) Hadithi iliyotajwa katika (a) (i) inatofautianaje na hadithi Nabawiy?

(i) Hadithi Qudusy mtume hueleza kama aliyoteremshiwa na Allah (s.w) ila Nabawiy hueleza kwa maneno yake mwenyewe.

(ii) Hadithi qudusy mtume hueleza kwa kuanza kusema "Allah (s.w) amesema..." ila Hadith Nabawiy Huanza kwa maneno yake


(iii) Hadithi Qudusy ni maneno ya Allah (s.w) ila Hadithi nabawiy ni maneno ya Mtume.

Kielelezo Na. 7.8: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Kipengele cha 7(c)

### 2.2.6 Swali la 8: Historia katika Uislamu.

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) kutoka katika mada ya Historia katika Uislamu, mada ndogo ya Historia ya Mitume walioteuliwa. Katika kipengele cha 8 (a) mwanafunzi alitakiwa kubainisha dhambi kubwa tatu zilizosababisha kuangamia kwa watu wa Lut (A.S). Katika kipengele cha 8(b) mwanafunzi alitakiwa kupendekeza njia mbili za kuiepusha jamii na adhabu walizopata watu wa Lut (A.S). Katika swali hili wanafunzi walipimwa umahiri wao katika kutathmini matukio ya kihistoria na namna ambavyo jamii ya sasa inaweza kuyazingatia.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu walifanya swali hili. Kati yao wanafunzi 50,689 (57.93%) walipata alama 2.5 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi 28,924 (33.06%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu, na wanafunzi 7,889 (9.01%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 8 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 8**. *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 8.*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 66.94 ya wanafunzi walipata kati ya alama 2.5 hadi 10 ikilinganishwa na asilimia 33.06 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 hadi 2).

Wanafunzi waliofaulu katika swali hili walionesha kuwa mahiri katika mada ya Historia katika Uislamu na walielewa vema matakwa ya kila kipengele cha swali hili. Aidha, katika kipengele cha 8(a) wanafunzi hao waliweza kubainisha dhambi kubwa walizozifanya watu wa Lut (A.S) kwa ufasaha kama vile; *(i) Walikuwa wakiwaendea wanaume wenzao katika kutosheleza matamanio ya ngono, (ii) Walikuwa wakifanya uharamia na uporaji wa mali za watu, (iii) Walikuwa wakifanya mambo maovu hadharani na kujifaharisha.* Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi aliyefaulu katika kipengele cha 8(a).

8. (a) Bainisha dhambi kubwa tatu zilizosababisha kuangamia kwa watu wa Lut (A.S).

(i) Waume Kuingiliana wenyewe kwa wenyewe

(ii) Kufanya maovu hadharani

(iii) Ubake na Kupora mali za watu.

Kielelezo Na. 8.1 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 8(a).

Kadhalika, katika kipengele cha 8(b); wanafunzi hao walipendekeza njia mbalimbali za kuiepusha jamii na adhabu kama walizopata watu wa Lut (A.S) kama vile; *(i) Kuacha kufanya maovu ya aina zote, (ii) Kufanya juhudi ya kuamrishana mema na kukatazana kufanya maovu, (iii) Wanajamii wanapaswa wasipende dunia kupitiliza wakumbuke na siku ya mwisho, (iv) Tujitahidi kusimamisha Uislamu wetu kwa mali na nafsi zetu (v) Tuwafate na kuwatii viongozi wetu wanapotuamrisha mema.* Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

(b) Pendekeza njia mbili za kuiepusha jamii na adhabu walizopata watu wa Lut (A.S).

(i) Kujiepusha na mambo maovu na mabaya


(ii) Kwa Kurudi Kwa aliyetuumba na kuomba msamaha

Kielelezo Na. 8.2 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Kipengele cha 8(b).

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali hasa katika kipengele cha 8(a). Wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhambi kubwa zilizosababisha kuangamia kwa watu wa Lut (A.S). Hivyo, hawakuweza kujibu swali ipasavyo.

Katika kipengele 8(a); wanafunzi hao waliorodhesha makosa mbalimbali kama vile; *(i) Kwa kumuasi Allah (S.W), (ii) Kwa kufanya tendo la jimai mchana wa Ramadhani, (iii) Kwa kufanya matendo asiyofanya Allah (S.W).* Wengine walijibu*; (i) Muhimu kuwa wasiri mwanzo, (ii) Ili waislamu wafanikiwe ili kazi kulingania*. Pia wengine walijibu*; (i) Kushirikana na kumfata shetani, (ii) Kumuiga Mtume, (iii) Kufanya vitu visivyoruhusiwa na Allah (S.W).* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kabisa kuhusu historia ya watu wa Nabii Lut (A.S).

Wengine walichanganya matukio (makosa) katika historia ya Bara Arab Zama za Jahiliyah na historia ya watu wa Nabii Lut (A.S) nao waliandika; *(i) Kuwauwa wanawake, (ii) Kuwazika watoto wa kike wakiwa hai, (iii) Kuwafanya wanaume kama warithi wa mali.* Majibu haya yaliashiria kuchanganya matukio katika historia ya jamii mbili tofauti. Kielelezo Na. 8.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 8(a).


8. (a) Bainisha dhambi kubwa tatu zilizosababisha kuangamia kwa watu wa Lut (A.S).


(i) zilizosababisha kuangamia kwa watu wa lut

(ii) njia mbili za kuiepusha Jamii na adhabu walizopata

(iii) ....................

Kielelezo Na. 8.3 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Kipengele cha 8(b).

Katika kipengele 8(b); baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walitoa hoja ambazo zilikuwa kinyume na matakwa ya swali. Baadhi ya hoja hizo ni*; (i) Ni njia ya kufikia uchamungu kwa wepesi, (ii) Kusamehewa swala kwa mja mzito.* Wengine waliandika kama vile*; (i) Kutumia muda mrefu msikitini, (ii) Mavazi na mwendo wake.* Pia wapo waliojibu; *(i) Kutomfuata Mwenyezi Mungu, (ii) Kuepuka kwa masanamu.* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu mada ya Historia katika Uislamu Kielelezo Na. 8.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.


(b) Pendekeza njia mbili za kuiepusha jamii na adhabu walizopata watu wa Lut (A.S).

(i) pendekeza za kuiepusha na watu lut.


(ii) Thalga ukutoa wa katika ya uhatga.

Kielelezo Na. 8.4 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Kipengele cha 8(b).

### 2.2.7 Swali la 9: Bara Arab Zama za Jahiliyyah Karne ya 6 A.D

Swali lilitolewa katika mada ya Bara Arab Zama za Jahiliyyah katika mada ndogo ya Kulingania Uislamu Makkah, ambapo mwanafunzi alitakiwa kutoa mafunzo matano kwa jamii ya sasa yanayotokana na Mtume (S.A.W) kulingania Uislamu Makka. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutathmini mafunzo muhimu yanayopatikana katika historia ya juhudi za Mtume (S.A.W).

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kati yao, wanafunzi 48,402 (55.32%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 23,216 (26.53%) walipata alama 2.5 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 15,884 (18.15%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 9 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 9:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9.*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa swali lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani asilimia 44.68 ya wanafunzi walipata alama 2.5 hadi 10 ikilinganishwa na asilimia 55.32 ya wanafunzi waliopata alama za chini (0 hadi 2).

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi waliopata alama za chini umeonesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Historia ya Mtume (S.A.W) akiwa Makka na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao walieleza tabia na kazi za Mtume (S.A.W) kabla ya kupewa utume kama vile: *(i) Alifanya kazi ya kuchunga mbuzi, (ii) Alikuwa akifanya biashara, (iii) Alikuwa mtunza hazina za watu.* Wengine walitaja nguzo za Uislamu kama vile: *(i) Kusimamisha Swala, (ii) Kufunga mwezi wa Ramadhani, (iii) Kutoa Zaka kwa waislamu, (iv) Kwenda Kuhiji Makka kwa wenye uwezo.* Kadhalika, mwanafunzi mwingine alichanganya nguzo za Imani na njia anazotumia Allah (S.W) kuwasiliana na waja wake kama vile: *(i) Kumuamini Allah (S.W), (ii) Kuamini Malaika wake, (iii) Kuamini Vitabu vyake, (iv) Kuamini Mitume wake, (v) Kuamini Qadar.* Majibu haya yanaonesha wazi kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu mafunzo yanayotokana na Mtume (S.A.W) kulingania Uislamu Makka. Hivyo, walikuwa wakiandika matukio mbalimbali katika maisha ya Mtume (S.A.W) ambayo baadhi ni ya kweli na mengine sio ya kweli.

Wengine walionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali hilo na kutaja changamoto mbalimbali alizokutana nazo Mtume (S.A.W) akiwa Makka kama vile; *(i) Makafiri walimkatisha Mtume tamaa, (ii) Makafiri walimhonga na kumrubuni Mtume (S.A.W), (iii) Makafiri walimtishia Mtume, (iv) Makafiri walitaka kumuua Mtume (S.A.W).* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa muktadha wa swali ambapo mwanafunzi alitakiwa kubainisha mafunzo yanayotokana na Mtume (S.A.W) kulingania Uislamu Makka. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

9. Mtume Muhammad (S.A.W) alifanya kazi kubwa katika kulingania Uislamu Makka. Toa mafunzo matano kwa jamii ya sasa kutokana na kazi hiyo.

(i) Watu wanamuabudu allah.

(ii) Watu wanasoma Quran.


(iii) Watu wanafunga mwezi mtukufu wa Ramadhani.

(iv) Watu wanatoa Zakka.

(v) watu wanahijji kwa wenye uwezo.

Kielelezo Na. 9.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Swali la 9

Wanafunzi waliofaulu katika swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya kulingania Uislamu Makka na walielewa vema matakwa ya swali hivyo, waliweza kubainisha mafunzo yanayopatikana katika jamii ya sasa kutokana na kazi hiyo aliyoifanya Mtume (S.A.W). Miongoni mwa mafunzo waliyoyatoa ni pamoja na; (i) *Hatunabudi kulingania Uislamu, (ii) Hatunabudi kuwa na subra katika kusimamisha Uislamu, (iii) Hatunabudi kutomuogapa yoyote isipokuwa Allah (S.W), (iv) Kumtanguliza na kumtegemea Allah (S.W) kwa kila jambo (v) Kuwa wakweli na waadilifu.* Kielelezo Na 9.3 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 9.


9. Mtume Muhammad (S.A.W) alifanya kazi kubwa katika kulingania Uislamu Makka. Toa mafunzo matano kwa jamii ya sasa kutokana na kazi hiyo.

(i) Kuwa na subra juu ya yale yatakayokupata ikiwemo na adhabu, njaa.
(ii) Kumtanguliza Allah na kumtegemea Allah kwa kila jambo.
(iii) Unajitunza pia kuanza kuwalingania kwanza watu wa familia yako.
(iv) Kuwa mkweli, muadilifu na kutunza amana na ahadi za watu.
(v) Kuwa mjuzi katika ulinganiaji ili kuudi makafiri wasijue mbinu mnazozitumia.

Kielelezo Na. 9.3 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 9


## 2.3 Sehemu C: Insha

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la insha kutoka katika mada ya Nguzo za Uislamu. Swali hilo lilikuwa na alama 15.

### 2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu

Swali lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu, katika mada ndogo ya Zaka, ambapo mwanafunzi alitakiwa kueleza tofauti baina ya Zaka na Sadaka. Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi kuchambua dhana ya Zaka na Sadaka kama inavyobainishwa katika Uislamu.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 87,502 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 31,156 (35.61%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 28,973 (33.11%) walipata alama 4.5 hadi 9 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 27,373 (31.28%) walipata alama 8.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wastani kwa wanafunzi katika swali la 10, kwani asilimia 64.39 ya wanafunzi hao walipata alama 4.5 hadi 15 ikilinganishwa na asilimia 35.61 ya waliopata alama za chini (0 hadi 4).

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wanafunzi waliofaulu katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Nguzo za Uislamu hususani katika mada ndogo ya Zaka na Sadaka na walielewa vema matakwa ya swali. Miongoni mwa tofauti walizobainisha ni pamoja na; *Zaka ya mali ya biashara na mifugo hutolewa baada ya kupindukia mwaka na mazao ya shambani hutolewa wakati wa mavuno lakini Sadaka hutolewa wakati wowote ambao mtu anapohitaji, Zaka hutolewa kwa waislamu tu lakini Sadaka hutolewa kwa yeyote bila ya kujali dini yake, Zaka hutolewa na tajiri lakini sadaka hutolewa na mtu yeyote, Zaka ni faradhi lakini Sadaka ni Sunnah iliyokokotezwa, Zaka ina kiwango maalumu lakini Sadaka haina kiwango maalumu, Zaka hutolewa mali tu lakini Sadaka hutolewa mali au huduma.* Hoja hizi zilibainisha wazi tofauti iliyopo baina ya Zaka na Sadaka katika Uislamu. Kielelezo Na 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

10. Kwa kutumia hoja tano, eleza tofauti baina ya Zaka na Sadaka katika Uislamu.

Zaka ni sehemu ya mali ya mtu ya kao ya mali ambacho anatakiwa kutoa zaka katika dini ya kiislam. ambayo anatakiwa kuwapa watu wanaostahiki na kwa waislam tu. lakini sadaka ni msaada anaopewa mtu kwa anayehitajia. sadaqa hutolewa kwa kiwango chochote ambacho muislam anacho. ufuatao ni utofauti kati ya zaka na sadaqa.

Zaka hutolewa baada ya mavuno lakini sadaka hutolewa wakati wowote ambao muislam anahitajia. zaka huweza kutolewa baada tu ya mavuno ya zao fulani mfano mahindi kama muislam amefikia nisaab basi ni wajibu kutoa za kwa watu wanaostahiki ambao ni waislam. wakati sadaka hutolewa muda wowote laki hutolewa kwa kila mtu.

Zaka hutolewa kwa watu waislam tu. lakini sadaka hutolewa kwa yeyote bila kujali dini anayotoka. Ingawa sadaka hutolewa kwa watu wanaostahiki tu kama wale wanaopewa zaka lakini hutolewa kwa dini zote lakini zaka hutolewa kwa watu wanaostahiki lakini kwa walio waislam kwa hiyo hatuna budi kujua tofauti hizi.

Zaka hutolewa na watu wenye mali tu. lakini sadaka Inajihusisha na utoaji wa huduma. tunafahamu kwa kutoa zaka ni nguzo ya tatu katika dini ya kiislam. kwa hiyo hatuna budi kutoa mali tulizotunukiwa na allah ambaye ndiye aliyeumba sisi sote kwa kututofautisha kwa mali.

Zaka ni faradhi lakini sadaka ni sunnah iliyokokotezwa. Ina maana kwa kutoa zaka ni lazima kwa kila aliyefikia kiwango lakini sadaka ni sunnah ambayo ukitoa unapata thawabu na usipotoa hupati dhambi pia zaka isipotolewa kwa wale waliofikia kiwango hupata dhambi na hasara nyingi katika maisha yao kwa mfano kuuguwa kwa magonjwa yasiyo na tiba. kutopewa msamaha na allah (s.w.) siku ya mwisho.

Zaka ina kiwango maalum. lakini sadaka haina kiwango maalum. Ina maana kwa muislam anapotaka kutoa zaka basi ni muhimu kujua kiwango maalum ambacho muislam anatakiwa kutoa. pia zaka kama haijafikia kiwango maalum basi hiyo huwa sio zaka bali ni sadaka. kwa hiyo muhimu kujua kiwango. lakini pia waislam wanaotaka kutoa sadaka. kwamba fahamu kuwa swadaka haina kiwango maalum. kilichowekwa. bali sadaka hutolewa na kulingana na uwezo wa mtoaji.

kwa ujumla. kuna utofauti mkubwa kati ya zaka na sadaka hivyo basi waislam hatuna budi kutekeleza na kusimamisha nguzo ya tatu ya uislam ipasavyo ili kuepuka madhara yatokanayo na kutokutoa huko. kutokana na kujua hayo yote pia tunatakiwa kutoa kwa wanaostahiki kama vile fukara, masikini, wasafiri na wengineo lakini

Kielelezo Na 10.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 10.

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi umeonesha kuwa, wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Zaka na Sadaka na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Aidha, baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kujenga hoja zinazobainisha tofauti kati ya Zaka na Sadaka, ingawa waliashiria kuelewa swali na kuwa na ufahamu kuhusu mada husika.

Baadhi ya wanafunzi ambao walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Zaka na Sadaka, walitoa hoja kama vile: *Zaka ni aina ya Sadaka ambayo hutolewa mwezi hadi mwezi lakini sadaka ni kujitolea kitu au pesa.* Mwanafunzi mmoja alieleza; *Zaka ni kitendo cha kuchangia kitu fulani kama vile majengo ya msikitini lakini Sadaka ni kitu chochote kinachopatikana katika njia ya halali na isiyo ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu.* Mwanafunzi mwingine aliandika; *Zaka inategemeana na kitu au wanyama pamoja na idadi na mwezi huo, kwa mujibu wa sheria ya kutoa zaka hiyo mfano una mbuzi 300 unatakiwa kutoa 02, na Sadaka hutolewa kwa kiasi chochote ila kisiwe cha kiwango kikubwa sana.* Hoja hizi hazikuwa sahihi hivyo walipata alama hafifu. Zaidi ya hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika; *Zaka ni kwenda kwenye Zaka lakini Sadaka ni mchango unaochangishwa msikitini, Zaka ni kutoa hela na kuteremsha mashamba lakini Sadaka ni kitendo cha kutoa hela sehemu yeyote panapouliza.* Mwingine akaandika; *Nia, Kusikiliza Qur'an na mavazi*. Kwa ujumla hoja hizi zinaonesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Zaka na Sadaka.

Mwingine alieleza umuhimu wa Sadaka badala ya kutofautisha na Zaka, nae alitoa hoja kama vile: *Kwa mfano Sadaka msikitini husaidia kuongeza au kununua vitu ambavyo havikuwepo mfano maiki, majeneza, baadhi ya sehemu ambazo hazijamaliziwa kujengwa, husaidia watu wasiojiweza, husaidia kipato msikitini.* Majibu haya yalionesha kuwa mwanafunzi hakuelewa matakwa ya swali hivyo, alitoa hoja ambazo hazikujibu swali hisika.

Mwanafuzi mwingine alichanganya sifa za Zaka na kuzieleza kama Sadaka, na Sadaka kuielezea kama Zaka. Mwanafunzi huyo aliandika; *Zaka haina muda maalumu ata sasa unaweza kutoa mfano njiani, nyumbani, msikitini, lakini Sadaka huwa na muda maalumu, Zaka hutolewa chochote ulichokuwa nacho hapo mfano mbuzi, ng'ombe,*

*ngamia, au hata mazao uliyovuna. Lakini Sadaka hutolewa kiwango au kitu maalumu kama inavyotakiwa.* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa sababu yalikuwa kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo namba 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 10.

10. Kwa kutumia hoja tano, eleza tofauti baina ya Zaka na Sadaka katika Uislamu.

Zaka ni aina ya sadaka ambayo hutolewa mwezi hadi mwezi na mtu anatoa 1/4 ya mali zake kwa watu na Sadaka ni kujitolea kitu, au pesa kwa watu wenye uhitaji na hutolewa siku na muda wowote. Zifuatazo ni tofauti baina ya Zaka na Sadaka katika Uislamu.

Kwanza, Zaka hutolewa kila mwisho wa mwezi na mtu na anatoa sawa kwa wote wata kao sitakoza kwake, wakati Sadaka ni kumpa mtu kitu au pesa anapohitaji kwa kujitolea kwa moyo mmoja mfano: Mtu katoka msikitini au kazini akakutana na mlemavu na akaombwa msaada na kutowa kwa moyo mmoja.

Pili, Zaka inategemeana na kitu au wanya ma pamoja na idadi na mwezi huwa, kwa mujibu wa sheria ya kutoa zaka hiyo mfano unambuzi 300 unatakiwa kutoa 2 na sadaka hutolewa kwa kiasi chochote ila kisiwe cha kiwango kikubwa sana.

Tatu, Zaka

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 10

Katika kielelezo Na. 10.2 mwanafunzi ameshindwa kubainisha tofauti sahihi ya Zaka na Sadaka katika Uislamu. Hivyo alijitungia hoja ambazo sio za kweli.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Katika upimaji huu mada zifuatazo zilihusika; *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Qur'an (86.11%) Nguzo za Uislamu (75.12%), Historia Katika Uislamu (66.94%), Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini (49.11%), Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (45.46%), Bara Arab zama za Jahiliyyah (44.68%), Sunnah na Hadithi (17.15%),* na *Kumjua Mwenyezi Mungu (6.43%).*

Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya wanafunzi kwa mada umeonesha kuwa kiwango kizuri cha ufaulu kilikuwa katika mada za *Qur'an (86.11%), Nguzo za Uislamu (75.12%)* na *Historia Katika Uislamu (66.94%)*. Vile vile kulikuwa na ufaulu wa wastani katika mada za *Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini (49.11%), Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (45.46%)* na *Bara Arab zama za Jahiliyyah (44.68%)*. Aidha, mada ambazo zilikuwa na ufaulu dhaifu zilikuwa *Sunnah na Hadithi (17.15%)* na *Kumjua Mwenyezi Mungu (6.43%)* ambazo zilipimwa katika maswali ya 3 na 7.

Ufaulu mzuri katika mada za *Qur'an (86.11%), Nguzo za Uislamu (75.12%)* na *Historia Katika Uislamu (66.94%)* ulichangiwa na maarifa mazuri waliokuwa nayo wanafunzi katika mada hizo, umahiri wao katika kubaini matakwa ya maswali na uwezo mzuri wa kuwasilisha majibu stahiki kwa ufasaha.

Ufaulu wa wastani katika mada za *Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini (49.11%), Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (45.46%)* na *Bara Arab zama za Jahiliyyah (44.68%)* ulisababishwa na wanafunzi kujibu maswali kwa kutoa baadhi ya hoja sahihi na kushindwa hoja zingine. Hali hiyo iliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika.

Aidha, ufaulu dhaifu katika mada za *Sunnah na Hadithi (17.15%)* na *Kumjua Mwenyezi Mungu (6.43%)* ulisababishwa na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na kushindwa kubaini matakwa ya maswali. Takwimu za ufaulu wa kila mada zimeoneshwa kwenye kiambatisho ambapo rangi nyekundu inaashiria kiwango cha chini cha ufaulu, rangi ya njano inaashiria kiwango cha wastani cha ufaulu. Kadhalika, rangi ya kijani inaonesha kiwango kizuri cha ufaulu.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu katika upimaji huu wa Kidato cha Pili (FTNA) 2023 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kilikuwa kizuri kwa asilimia 68.32. Uchambuzi huu umeonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango hicho katika upimaji unaofuata. Changamoto zilizojitokeza kwa wanafunzi katika kujibu maswali ni pamoja na kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza, kushindwa kubaini matakwa ya swali na kukosa maarifa katika mada mbalimbali hususani mada za *Sunnah na Hadithi (17.15%)* na *Kumjua Mwenyezi Mungu (6.43%)*.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wawaongoze wanafunzi kujadili katika vikundi na kurejea muhtasari wa somo na vitabu vya kiada na ziada ili kupata maarifa ya kutosha hususani katika mada za *Sunnah na Hadithi* na *Kumjua Mwenyezi Mungu.*

(b) Walimu wawapime wanafunzi kwa maswali yanayopima ngazi za juu za umahiri ili kuwajengea uwezo wa kubaini matakwa ya swali na namna bora ya kuwasilisha majibu (hoja).

**Kiambatisho Cha Pekee**

**Uchambuzi wa Ufaulu wa Wanafunzi Katika Mada**

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Wanafunzi Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1 | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunna na Hadithi, Historia Katika Uislamu. | 1 | 86.51 | 86.51 | Vizuri |
| 7 | Qur'an | 6 | 86.11 | 86.11 | Vizuri |
| 4 | Nguzo za Uislamu | 2 | 85.85 | 75.12 | Vizuri |
| | | 10 | 64.39 | | |
| 6 | Historia Katika Uislamu | 8 | 66.94 | 66.94 | Vizuri |
| 3 | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini | 4 | 49.11 | 49.11 | Wastani |
| 5 | Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu | 5 | 45.46 | 45.46 | Wastani |
| 8 | Bara Arab zama za Jahiliyyah | 9 | 44.68 | 44.68 | Wastani |
| 9 | Sunnah na Hadithi | 7 | 17.15 | 17.15 | Dhaifu |
| 2 | Kumjua Mwenyezi Mungu | 3 | 6.43 | 6.43 | Dhaifu |